

Muhtasari wa Mwenendo wa Mvua kwa Siku 10 Zilizopita na Matarajio kwa siku 10 Zijazo

1.0 MUHTASARI WA MWENENDO WA HALI YA HEWA KWA TAREHE 11-20 JUNI, 2026 NA MATARAJIO YA HALI YA HEWA KWA TAREHE 21-30 JUNI, 2026.

1.1 MUHTASARI WA MWENENDO WA VIASHIRIA NA MIFUMO YA MVUA TAREHE 11-20 JUNI, 2026.

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliendelea kuimarika wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) iliendelea kudhoofika. Hali hii ilisababisha ukanda mvua kuendelea kusogea kuelekea kaskazini zaidi nje ya nchi yetu. Vilevile, upepo wa bahari wenye unyevunyevu uvumao kutoka mashariki na kuelekea katika maeneo ya ukanda wa pwani uliimarisha kwa vipindi mifumo isababishayo mvua katika maeneo ya ukanda wa pwani na maeneo jirani hususan yale yaliyopo nyanda za juu kaskazini mashariki.

1.2 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 11-20 JULI, 2026.

Viashiria vilivyotajwa hapo juu vilipelekea vipindi vya mvua katika maeneo ya ukanda wa pwani na yale ya nyanda za juu kaskazini mashariki.

2.0 MATARAJIO YA HALI YA HEWA KWA TAREHE 21-30 JUNI, 2026.

2.1 VIASHIRIA NA MIFUMO YA MVUA KWA TAREHE 21-30 JUNI, 2026.

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) inatarajiwa kuendelea kuimarika wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) inatarajiwa kuendelea kudhoofika. Hali hii inatarajiwa kusababisha ukanda mvua kuendelea kusogea kuelekea kaskazini zaidi nje ya nchi yetu. Vilevile, upepo wa bahari wenye unyevunyevu uvumao kutoka mashariki na kuelekea katika maeneo ya ukanda wa pwani unatarajiwa kuimarisha kwa vipindi mifumo isababishayo mvua katika maeneo ya ukanda wa pwani na maeneo jirani hususan yale yaliyopo nyanda za juu kaskazini mashariki.

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,
Kiwanja Na. 6, Kitalu "N", Mtaa wa Fahmida, Dodoma jiji,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe: met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

2.2 MWELEKEO WA HALI YA HEWA KWA TAREHE 21-30 JUNI, 2026.

Kanda ya ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara): Hali ya ukavu kwa ujumla inatarajiwa.

Nyanda za juu kaskazini-mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro): Vipindi vya mvua nyepesi vinatarajiwa katika maeneo machache.

Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba): Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache.

Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora): Hali ya ukavu inatarajiwa.

Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida): Hali ya ukavu inatarajiwa.

Nyanda za juu Kusini-magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa): Hali ya ukavu kwa ujumla inatarajiwa.

Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi): Hali ya ukavu kwa ujumla inatarajiwa.

Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro): Hali ya ukavu kwa ujumla inatarajiwa.

Imetolewa na:

MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,
Kiwanja Na. 6, Kitalu "N", Mtaa wa Fahmida, Dodoma jiji,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz